



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.MM/AR/ S20/12/6

16.02.2022

TANGAZO NAFASI ZA AJIRA ZA MUDA

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Arusha anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa zinazohitajika na wenye nia ya kufanya kazi ya zoezi la Anwani za Makazi katika Kata na Vijiji vya Halmashauri ya Arusha, kuomba nafasi hizo.

A. SIFA ZA MWOMBAJI:

1. Awe ni Raia wa Tanzania.
2. Awe amemaliza Kidato cha nne na kuendelea.
3. Ajue kusoma na Kuandika.
4. Anamiliki simu janja yenye sifa ya **Android 7** na uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
5. Awe na uwezo wa kutumia simu Janja.
6. Awe na Akili timamu.
7. Awe na barua pepe (email) na nywila (password) inayofanya kazi.

B: KAZI NA MAJUKUMU:

1. Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
2. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
3. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba na maeneo ya huduma kwa kutumia Mfumo wa Anwani za Makazi.
4. Kutuma Data kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi.

C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA:-

1. Nakala ya cheti cha Kidato cha nne na cheti cha taaluma.
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Picha (Passport size 2).
4. Weka namba zako za simu zinazopatikana muda wote.

D. MALIPO:

- Malipo ya ajira ni Tsh. 10,000/= kwa siku.

E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI:


1. Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba za simu na barua pepe (email).
2. Barua ya maombi ipitishwe kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji husika na kuwasilisha kwa Mtendaji wa Kata.
3. Mwombaji anashauriwa kuomba nafasi kwenye Kata anayoishi.

F. MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUWANI IFUATAYO:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Arusha,
S.L.P. 2330,
ARUSHA.**

G. TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24.02.2022 saa 09:30 Alasiri.



Selemani H Msumi.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)